



MACHAKOS UNIVERSITY COLLEGE

(A Constituent College of Kenyatta University)
University Examinations for 2013/2014

SCHOOL OF EDUCATION

DEPARTMENT OF LINGUISTICS AND LANGUAGES

Examination for Diploma in Education

AKS 0103: HISTORIA YA KISWAHILI

Date: 30/7/2014

Time: 11:00 -

MAAGIZO

JIBU MASWALI MATATU; SWALI LA KWANZA NI LA LAZIMA

1.
 - (a) Kwa kurejelea hoja sita, dhihirisha kuwa kiswahili ni lugha ya kibantu. (alama 12)
 - (b) Kuna umuhimu gani kujifunza kazi hii kwa mwanafunzi wa Kiswahili. (alama 8)
 - (c) Thibitisha kauli hizi
 - (i) Kiswahili ni lugha ya kiarabu
 - (ii) Kiswahili ni lugha mseto (alama 10)
2. Mambo yafuatayo yalisaidia vipi kukua na kuenea kwa kiswahili?
 - (a) Ndoa kati ya waarabu na wanawake wa kibantu
 - (b) Biashara
 - (c) Hati za kiarabu
 - (d) Dini ya kiislamu
3. Kwa nini ushahidi ufuatao kuhusu chimbuko la kiswahili si kweli? (alama 20)
 - (i) Kiswahili ni mojawapo ya lahaja za lugha ya kiarabu
 - (ii) Kiswahili kimekopa sana maneno kutoka lugha ya kiarabu
 - (iii) Kiswahili ni zao la ndoa kati ya waarabu na wanawake wa kibantu
 - (iv) Miji ya uswahili imestawishwa na kuimarishwa na wageni waliotembelea upwa wa pwani ya mashariki
4. Fafanua mchango wa wamishenari na walowezi katika ukuzaji na usambazaji wa Kiswahili bara la nchi za Afrika mashariki (alama 20)
5. Eleza jinsi misafara ya waarabu na biashara zilivyochangia katika uenezaji wa Kiswahili. (alama 20)